

HALMASHAURI YA MJI TUNDUMA

(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi wa Mji)



Ofisi ya Mkurugenzi
P. O. BOX. 73,
TUNDUMA -SONGWE.

FAX NO. 025-253023

Email: tundumatcouncil@yahoo.com

04/04/2018

Kumb.Na. TTC/01/94/6

TANGAZO LA KAZI

(NAFASI ZA AJIRA YA MKATABA KWA KADA ZA AFYA)

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Tunduma anawatangazia wananchi wote wenye sifa kuomba kujaza nafasi 11 za ajira kwa kada za Afya kama zilizoorodheshwa katika Tangazo hili.

1.0: Afisa Tabibu Daraja II (CO) – NAFASI 3

1.1: *Sifa mahsusi za kuajiriwa kwa nafasi hii*

Awe amehitimu Elimu ya Kidato cha Nne/Sita na kufuzu mafunzo ya utabibu (Clinical Medicine) ngazi ya Stashahada katika chuo kinachotambuliwa na Serikali.

Mshahara kwa mwezi TShs. 500,000

1.2: KAZI NA MAJUKUMU

1. Kutambua na Kutibu wagonjwa wa kawaida
2. Kusimamia utendaji wa watumishi walio chini yake
3. Kufanya upasuaji mdogo
4. Kushiriki kupanga na kutekeleza huduma za afya ya msingi
5. Kuelimisha jamii na kutoa ushauri nasaha kwa wagonjwa
6. Kushauri na kuhamasisha wananchi kuchangia huduma za afya na mfuko wa afya ya jamii
7. Kuweka kumbukumbu za vifaa na zana za kutolea huduma
8. Kuandaa na kutoa taarifa za utekelezaji wa shughuli za kituo
9. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi

2.0: MUUGUZI II (NURSE II)- NAFASI 5

2.1: *Sifa Mahsusi za Kuajiriwa kwa nafasi hii*

Awe amehudhuria na kufuzu mafunzo ya Uuguzi na Ukunga (Nursingi and Midwifery training) ngazi ya cheti (astashahada) katika

